EDUCATION AND ENVIRONMENT PROMOTERS GROUP

ST. JAMES KIGOMA SECONDSARY SCHOOL

REG. NO: S.4363, CENTRE NO:S. 4516

P.O.BOX 1325 KIGOMA. Mobile: 0755093324

MWANAFUNZI.............................................................................................

S.L.P.........................................................................................................

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO</u>

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha TANO mwaka 2024/2025 katika tahasusi (combination) ya **HGL, HGK ,HKL, HGE, EGM, CBG, PCB & PCM.** Shule hii ipo mjini kigoma eneo la Mlole mkabala na ofsi za SIDO mkoa, jirani na nyumba mpya za shirika la nyumba la Taifa (NHC), pia inapakana na shule ya sekondari Masanga.

Kwa wanaotoka mikoani au nje ya manisipaa ya Kigoma – Ujiji wakishuka stand mpya ya mabasi wafuate barabara iendayo mjini wakifika SIDO wavuke barabara upande wa kulia watafika shuleni ndani ya dakika tano.

Ni shule ya BWENI na KUTWA kwa wavulana na wasichana kuanzia kidato cha kwanza I hadi kidato cha sita VI.masomo ya PRE- FORM FIVE yataanza tarehe 03/06/2024 hadi tarehe 30/06/2024 kwa gharama ya Tshs. 50,000/= (elfu hamsini tu). Muhula wa masomo utaanza tarehe 08/07/2024.wanafunzi wa BWENI wanatakiwa kufika shuleni tarehe 06/07/2024 kabla ya saa 11:00 jioni.

## 1.0 SARE YA SHULE

A. WAVULANA

(I) Shati mbili nyeupe mikono mirefu na tai
(II) Suluali mbili rangi ya BLUU BAHARI (Light blue) isiyobana
(III) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba
(IV) Soksi rangi NYEUSI

B. WASICHANA

(I) Shati/ blauzi mbili mikono mirefu na tai
(II) Sketi mbili langi ya BLUU BAHARI yenye malinda **6** urefu hadi jicho la mguu
(III) Viatu vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi.
(IV) Soksi langi **NYEUPE**

## 2.0 VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULE.

- Rimu moja ya karatasi A4 kwa kila mwaka
- Ndoo moja ya lita kumi
- Ufagio mmoja
- Fyekeo au kwanja moja
- Sahani ,bakuli na kijiko kwa wanafunzi wote

## 3.0 GHARAMA ZA MASOMO

Gharama za masomo kwa mwaka wa kwanza ni jumla ya **Tshs.1,320000/=kwa BWENI** na kwa **KUTWA/DAY** ni **Tshs. 875,000/=** Fedha hiyo inaweza kulipwa kwa mkupuo mmoja, miwili au awamu nne kama ifuatavyo;

| | DAY | BWENI |
|---|---|---|
| Mwezi julai mwanzoni | 275,000/= | 420,000/= |
| Mwezi oktoba mwanzoni | 200,000/= | 300,000/= |
| Mwezi januari mwanzoni | 200,000/= | 300,000/= |
| Mwezi march | 200,000/= | 300,000/= |
| **Jumla kuu Tsh.** | **875,000/=** | **1,320,000/=** |

Malipo yote yapelekwe Benki katika akaunti namba 0150256138000 iliyopo CRDB jina la akaunti ni St. james kigoma sec. school, kisha mwanafunzi alete pay-in-slip(Risiti ya Bank) shuleni. Shuleni hatupokei fedha tasilim, hivyo kila mtu alipie malipo yote Benki.Baada ya malipo mwanafunzi afikapo shuleni atapatiwa vifaa vifuatavyo;

**BWENI** –T-Shirt 2na kitambulisho cha shule
**DAY** -T-Shirt 1na kitambulisho cha shule
**NB: Chakula cha mchana hutolewa kwa wanafunzi wote wa Bweni na Day/kutwa**

## 4.0 MAHITAJI YA MWANAFUNZI WA BWENI

- Godoro linapatikana shuleni.
- Uje na shuka mbili zenye langi ya blue
- Uje na vyombo vyakulia chakula sahani, bakuli ,kikombe na kijiko
- Uje na chandarua
- Uje nan doo lita 10na beseni kwa ajili ya usafi kuoga na kufulia
- Uje na nguo za michezo, Bukta kwa wavulana, na track suit ya blue kwa wasichana
- Uje na sketi mbili rangi nyeusi za kuvaa baada ya masomo kwa wasichana
- Kwa wavulana uje na suruali mbili rangi nyeusi za kuvaa baada ya masomo
- Uje na fedha ya matibabu yako binafsi isiyopungua tshs. 20,000/= na itunzwe kwa muhasibu wa shule.

## 5.0 SIFA ZA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO

Mwanafunzi yeyote aliefanya mthihani wa Taifa wa kuhitimu kidato cha NNE na kufaulu kwa daraja I,II,au III au aliepata C zisizopungua tatu katika masomo yake isipokua som( la Bible knowledge, EDK,Arabic na muziki

### SHERIA NA KANUNI MHIMU ZA SHULE HII.

Shule hii inaongozwa kwa mjibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Pia inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo kwa mda wote ukiwa Mwanafunzi wa shule hii.

(a) Kuwa na heshima kwa viongozin,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Kuwa na mahudhulio mazuri katika kila shughuli za darasani na nje ya darasa.
(c) Unatakiwa kuwahi shuleni na katika shughuli za shule utakazopewa
(d) Unapaswa kufaham mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu kuwepo shuleni wakati wa masomo .
(e) Unatakiwa kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule.
(f) Unatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shule.
(g) Unatakiwa kuhudhulia shule na kufanya mazoezi, majalibio na mithihani yote itakayotolewa na kuifaulu vizuri.
(h) Unatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Lugha ya mawasiliano na kufundishia ni kingeleza tu
(j) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi, au kusuka nywele kwa wasichana (twende kilioni mistari mitano) hairuhusiwa kunyoa mitindo kiduku,kipara n.k

***UFAULU***: Kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu mithihani na kupata daraja (Division) I,II au III, atakaye shindwa kufikia kiwango hicho hataruhusiwa kupanda darasa.

### MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama bangi, cocaine, kubeli n.k
5. Kupigana au kupiga
6. Kuhalibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudhalau bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi

13. Kutoroka Hosteli na kwenda nje ya shule bila ruhusa
14. Mwanafunzi kuja na simu ya mkononi shuleni
15. Kutofanya mthihani ya shule na ile ya nje ya shule kama Mock n.k
16. Kuchelewa kuripoti shule kwa mda wa Zaidi ya wiki moja

***NB: Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na kuyazingatia kikamilifu.***

Kwa ujumla Heshima (nidhamu) juhudi ya kazi na maarifa katika maisha ya shule ni msingi wa mafanikio. Atakaye kiuka mojawapo ya makosa hayo, hasa kutoroka Bweni/ shule, adhabu yake ni kusimamishwa masomo kwa mda wa wiki mbili , kulipa faini Tsh 100,000/= au kufukuzwa shule

**RATIBA YA MASOMO:**

Masomo huanza saa 2:00 Asubuhi kwa kila siku ya jumatatu hadi ijumaa hadi saa 9:30 alasili na 9:40 hadi saa 11:30 jioni. Siku ya jumapili ni ibada kuanzia sa 3:30 asubuhi hadi7:00 mchana. Ni muhimu kila mwanafunzi azingatie ratiba hiyo na kutii sheria zote za shule.

Kauli mbiu ya shule ***"ELIMU KWA MAENDELEO"***

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI ST. JAMES KIGOMA***

..............................

***MKUU WA SHULE***

HEADMASTER
ST. JAMES KIGOMA SEC. SCHOOL
P.O. Box 1325 KIGOMA